

MED CENTER HEALTH

SERA YA MSAADA WA KIFEDHA

Muhtasari wa Lugha

*Imerekebishwa
mnamo Septemba*

Med Center Health hutoa misaada ya kifedha kwa watu waliyotimiza masharti, wanaopata dharura na huduma nyingine za afya kutoka kwenye Hospitali za Taasisi ya Afya ya Commonwealth (CHC) na washirika wao wa moja kwa moja.

Lengo la Sera yetu ya Msaada wa Fedha ni kutambua njia ambazo CHC hufanya huduma bora za afya kupatikana, ambazo ni nafuu na zinapatikana kwa wote bila kujali uwezo wao wa kulipia.

SIFA ZA KUCHAGULIWA

Mpango wetu wa msaada wa kifedha unategemea ukubwa wa kaya na mapato ya kila mwaka kabla ya kodi. Ikiwa una bima ya kutosha, mapato au mali zinazopatikana kulipia huduma yako, huenda usistahili usaidizi wa kifedha.

Waombaji kwa usaidizi wa kifedha wanatakiwa kuomba kwenye programu za umma kwa ajili ya kushughulikiwa, ikiwa wanakidhi vigezo. Wagonjwa ambao hawatatoa ushirikiano katika kuomba kwenye programu ambazo zinaweza kulipa huduma zao za afya wanaweza kunyimwa msaada wa kifedha.

Kuna huduma nyingine ambazo hazitolewi msaada wa kifedha, ikiwa ni pamoja na, lakini sio tu kwa: huduma zisizohitaji dawa, upasuaji kwa ajili ya kubadilisha sura, upasuaji wa kupunguza unene na huduma nyingine kama zilivyoorodheshwa kwenye Sera ya Usaidizi wa Fedha.

WAGONJWA KWENYE WODI ZA DHARURA

Wagonjwa wanaotumia idara zetu za dharura hawatazingatiwa kwa usaidizi wa kifedha au taarifa ya malipo kabla ya utoaji wa taarifa ya uchunguzi wa matibabu na, kwa kiasi kikubwa, huduma zinazohitajika kutibu Mgonjwa au kumuimarisha kwa ajili ya uhamisho kama ilivyoainishwa.

NAMNA YA KUOMBA MSAADA WA KIFEDHA

- Wajulishe wafanyakazi wa CHC wakati au kabla ya wakati wa usajili kuwa wewe ni mgonjwa asiye na bima au bima yako haitoshi au anayehitaji msaada wa kifedha.
- Pakua na kuprint Programu ya Usaidizi wa Fedha kutoka kwenye tovuti ya CHC na utume fomu ya maombi kamil na viambatanisho vinavyohitajika kwenye anwani ya tovuti. Linki ya ukurasa wa Tovuti wenye Fomu ya maombi ni: <https://cfrbilling.com>.
- Omba Msaada wa Kifedha kwa simu: 800-786-1581 au 270-745-1100. Maombi ya Msaada wa Kifedha na Muhtasari wa Lugha(PLS) ya FAP utatumwa kwako, bila malipo.

SERA YA MALIPO

Ili kudhibiti gharama za huduma za afya na kutuwezesha kutumikia vizuri jamii yetu, malipo yanatarajiwa ndani ya siku 20 ya taarifa ya kwanza ya kulipia. Ikiwa huwezi kulipa kikamilifu wasiliana na ofisi yetu ya bili ili kujadili mipangilio ya malipo, tunatoa mipango mbalimbali ya malipo ili kukusaidia. Mpango wetu wa malipo unategemea jumla ya pesa ya dola kama deni kwa kila akaunti. Mipango ya malipo inaweza kuwa miezi mitatu hadi muda mrefu kama miezi 60. Tafadhali wasiliana na idara ya kulipa kwenye namba ya simu (270)745-1100 au 800-786-1581. Jumatatu hadi Ijumaa 8:00 - 4:30 jioni kwa

ANWANI YETU

Ikiwa una maswali yoyote, tafadhali wasiliana na ofisi yetu inayohusika na Bili kwenye namba ya simu (270)745-1100 au 800-786-1581, Jumatatu hadi Ijumaa 8:00 - 4:30 jioni. Maelezo yanapatikana pia kwenye www.cfrbilling.com